

HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI



UUZAJI WA VIWANJA KATIKA MANISPAA YA KIGAMBONI

Katika mpango wa kuhakikisha mji unapangwa kwa kufuata kanuni, taratibu na sheria za mipango miji, Mkurugenzi wa **Manispaa ya Kigamboni**, anawatangazia wananchi kuwa, anauza viwanja zaidi 6,000 vilivyopimwa vyenye matumizi mbalimbali vikiwemo Viwanda. Viwanja hivyo viko katika kata ya **Kisarawe II, Somangila, Kimbiji na Pembamnazi**.

- Fomu za maombi ya kumiliki kiwanja zitauzwa kwa **Tshs. 20,000/=** katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni zilizopo Mjimwema.
- Idadi ya fomu zitakazouzwa ni sawa na idadi ya viwanja vilivyopimwa.
- Waombaji ambao si raia wa Tanzania wanapaswa kupata kibali toka T.I.C
- Viwanja vyote vinafikika kwa urahisi. Aidha, Barabara zote za ndani ya mradi zimeshafunguliwa na baadhi vina miundombinu ya maji na umeme.
- Fomu za maombi ya kiwanja zitaanza kutolewa tarehe **18 - 25/04/2017** kuanzia **saa 3 asubuhi** hadi **saa 9 alasiri**.
- Mwisho wa kurudisha fomu ni tarehe 28/04/2017 saa 9 alasiri.

Imetolewa na:

Stephen E. Katemba
MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGAMBONI